

REPUBLIC OF KENYA
COUNTY ASSEMBLY OF KILIFI

THE HANSARD

Tuesday, 30th October, 2018

*The House met at the County Assembly Chamber,
Malindi Town, at 9.30 a.m.*

[The Deputy Speaker (Hon. Kenga) in the Chair]

PRAYERS

MOTION

GOVERNOR'S ADDRESS: EXPOSITION OF PUBLIC POLICY

The Leader of Majority (Hon. Mwathethe): Mr. Speaker, Sir, I would like to thank you this morning for giving me this chance to move this Motion on the First Address of the Second County Assembly by His Excellency, Amason Jeffah Kingi E.G.H., The Governor, Kilifi County on Wednesday, October 24th, 2018.

I would like to move a Motion:-

THAT, Pursuant to the provisions of Standing Order no. 20(5), the thanks of the County Assembly be recorded for the exposition of public policy contained in the First Address of the Second County Assembly by his Excellency, Amason Jeffah Kingi, E.G.H., The Governor, Kilifi County (Wednesday, 24th October, 2018), laid on the Table of this honourable House on Monday, 29th October, 2018.

This being a Government Motion, before I call the Chief Whip to second, I would like to make just a few remarks. Everybody was here when the Governor gave his speech for the first time in this Second Assembly. He articulated on several issues that I do not want to repeat because everybody heard and now I would call up on all Members to ventilate on the issues mentioned by the Governor. With those few remarks, I want to call on my colleague hon. Mwayaa to second.

(Hon. Mwayaa seconded)

(Question proposed)

Hon. Mwayaa: Asante mheshimiwa Spika. Nimesimama kuunga mkono hotuba ya Gavana aliyoisoma katika Bunge hili. Katika hotuba hiyo, Gavana aligusia mambo ya ufisadi na kusema katika serikali ya Kilifi, ameweka mikakati ya kutosha kuhakikisha ufisadi hauathiri Kilifi. Katika Bunge letu la kwanza, kulikuwa na hali ya sitofahamu na pesa zikapotea katika

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Kilifi. Kama wajumbe wa Kaunti hii tulifurahi kusikia kuwa kumewekwa mikakati ya kuzuia mambo kama hayo kufanyika.

Gavana pia alitaja mambo ya *maintenance* ama ukarabati wa magari. Kutakuwa na mahali pa kurekebisha magari yetu. Kwa sasa, ukienda katika gereji ndogo ndogo utaona magari ya Kaunti yakitoka huko. Ni jambo la kufurahisha kusikia kwamba kutatengwa sehemu ya gereji kwa magari ya Kaunti pekee. Kwa maoni yangu, hilo ni jambo zuri sana kwa sababu hutaona magari hasa kama ambulensi zikitapakaa hapa na pale.

Katika hotuba hiyo, pia aligusia mambo ya ujenzi wa hospitali unaoendelea pale Kilifi itakayokuwa kubwa ndani ya Kaunti...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes hon. Kiraga, what is your Point of Order?

Hon. Kiraga: Mr. Speaker, the Member on the Floor is the Chief Whip, so if he is highlighting any issue that was mentioned by the Governor, he should also expound. He is talking of the Governor giving out mechanisms on how to combat corruption; I have gone through his speech and I have not seen any mechanisms put in place to combat corruption can he explain further?

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Majority Whip, please proceed.

Hon. Mwayaa: Mheshimiwa Spika, nikisema kwamba Gavana alisema ataweka mikakati; sote tulikuwa hapa na akatamka kwamba mikakati imeshawekwa ya kuhakikisha kwamba pesa ya wana Kilifi haipotei. Ninashangaa kusikia mheshimiwa anauliza ni mikakati gani nikisimama ninasema yale...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): There is a Point of Information from hon. Member for Garashi, but before I give him an opportunity. Do you want to be informed?

Hon. Mwayaa: Anaweza akanijulisha tu, haina shida.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Proceed.

Hon. Ziro: Thank you Mr. Speaker. I am rising on a Point of Information to hon. Kiraga...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): You are out of order! You can only inform the Member who is on the Floor...

Hon. Ziro: Whatever I am talking about here is important to both of them, so I am informing hon. Mwayaa.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Proceed.

Hon. Ziro: If you look at the Governor's Speech on page five the second paragraph, I will start from the third last paragraph and I will read;

"My Government also intends to engage the World Bank on automation of additional revenue streams that are not covered in the Strathmore University automation initiative.

In an effort to address Revenue shortfalls and leakages on revenue streams outsourced to the private collection agent Raindrops Ltd., my government has placed government personnel at each collection centre to ensure transparency and accountability on the revenue collected through Raindrops Ltd. This has resulted into tremendous improvement in our daily collections of Cess and parking fees."

This is one of the steps that the Governor has taken to make sure that corruption is curbed in our County. I wanted to inform Members that there are steps that have been taken by the Governor.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Proceed Majority Whip.

Hon. Mwayaa: Asante mheshimiwa Spika, na ndio maana huyu Mheshimiwa wa Garashi tunamuita *samba*; yeye pia wakati Mheshimiwa Gavana akisoma alisikiza lakini inaonekana akili yake alikuwa ameituma mahali. Mikakati iliyowekwa itasaidia wana Kilifi na

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

hiyo ni miongoni mwa mambo mengi yaliyozungumzwa na Gavana wetu hapa. Naunga mkono hotuba hiyo.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Members who would wish to make their contribution, please there is a problem with the system from my side so please raise your hand. Yes hon. Member for Bamba Ward, please proceed.

Hon. Mwambire: Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia fursa hii kuweza kuchangia Hoja ama taarifa ambayo iliweza kupeanwa na Gavana siku ya tarehe 24 siku ya Jumatano. Mimi nataka kupongeza kwanza katika kifungu kile cha nne nikiwa mwanakamati wa Kamati ya Kilimo, Uvuvi na Ufugaji. Hapo katika hiyo Hotuba kama ilivyoandikwa niliona kwamba katika mchakato ule wa CIDP (County Integrated Development Plan) 2018/2019 tumeona kwamba ukulima, ufugaji na uvuvi, utaimarishwa katika Kaunti yetu ya Kilifi.

Jambo ambalo ni la kufarahisha ni kwamba Kilifi iko na ardhi nyingi ambayo inaweza kutumika kikamilifu ili kuona kwamba mambo haya yanatekelezeka na kuona kwamba wananchi wetu wa Kilifi wameinuka ki uchumi na pia ki miundo msingi wa kimaisha. Basi, ni kuomba tu kwamba Wabunge wenzangu tunapofikia mambo ya kupanga bajeti tuone kwamba sekta hii tumeiangazia kikamilifu maanake ndio sekta peke yake ambayo inaweza kubadilisha maisha ya mtu wa Kilifi.

Ukulima tunajua kwamba katika sehemu yetu tumebarikiwa. Tuko na misimu miwili ambayo huwa tunapata mvua katika Kaunti yetu ya Kilifi. Japo wakati mwingine tunapata mvua chache, lakini jambo la kufurahisha ni kwamba tumeona Gavana amepanga shilingi milioni 50 katika maeneo ambayo wakati mwingine tunapata mvua chache. Sehemu hizi huwa zinakabiliwa na ukame; fedha hizi zitahakikisha zimepata ile hali ya unyunyiziaji maji mashambani na pia kuona kwamba kuna maji ya kutosha mashambani kwa mifugo, wanadamu na kwa wakulima.

Kwa hivyo, biu hili linaweza likachangia zaidi hasa pale ambapo ninaona kuna uwekezaji wa *European Union* (EU) na lile shirika linaitwa TSS ambalo tayari limezuia ule mradi wa mambo ya mkorosho pale Kakanjuni. Basi itakuwa vyema zaidi sisi kama wabunge tunapokuwa na mikutano kule nyanjani tuweze kuwahamasisha wakulima ili waweze kupata miche na wapande mikorosho kwa wingi ili tuweze kurudi tena kama zamani ule wakati wa mkorosho ulipokuwa ukiwika Kilifi kama kiwanda ambacho kilikuwa kimeajiri watu wengi zaidi.

Nilipokuwa nikiendelea ni kwamba katika *projection* za wale ambao walijaribu kufanya ukarabati wa mradi waliona kwamba mradi huu utakapoteketezeka utaweza kupeana ajira ya zaidi ya watu 5,000. Pia nimeona mambo ya *simsim* na nikikumbuka Kilifi Kaunti miaka hiyo ya nyuma ya 1995 kurudi nyuma ilikuwa inaongoza kwa mambo ya *simsim production* na hata pia mambo ya uzalishaji wa pamba.

Nimeona kwamba mradi kama huu wa pamba ambao hapa Malindi *Municipality*, tulikuwa na ile inaitwa Malindi *ginners* ambayo ilikuwa ikichukua pamba kwa ajili ya kupeleka kwa vile viwanda vya kutengeneza nguo na magoro. Nimeona kwamba sehemu kama Magarini *Constituency* bado iko na *potential* ya kuweza kuzalisha hili pamba na kuzalisha *simsim*. Kwa hivyo, sisi kama Kamati ya Kilimo pamoja na Mwenyekiti wetu tumeona kwamba tunapokuwa na ushirikiano mzuri wa kuimarisha hii sekta kama maono ya Gavana na *Executive* vile iko, basi Kilifi itaimarika kiuchumi.

Lengine ambalo limenakiliwa katika hotuba hii ni mambo ya ufugaji. Hapa kuna sheria ambayo Gavana alikuwa anauliza kama tutaipisha; mambo ya *abattoirs*. Tunajua kwamba Kilifi inaongoza kwa mambo ya ufugaji. Hii ni njia ambayo itaweza kusaidia tukawa na *slaughter house* nzuri ambapo tutakuwa tunachinja ng'ombe ama mbuzi kwa wingi na hata tutaweza ku *export* hizi nyama kwa ajili ya kuboresha soko letu hapa.

Vile vile kuna ile mipango ya *Blue Economy Conference*; mambo ya uvuvi ambapo tuko na *stretch* ndefu sana ya... (*inaudible*) tuko na kilomita zaidi ya 264 za ufuo wa bahari ambao ninaamini kwamba Bunge hili litakapojizatiti na kuona kwamba tunatilia mkazo katika mambo haya, basi pia tunaweza kuwa na samaki wa kujitosheza pia tukawa na samaki ambao tunaweza ku *export* kwa ajili ya kuuza.

Kwa hivyo, mimi napongeza sana hii hotuba katika mrengo ule wa mambo ya kilimo na uvuvi. Pia nikiwa mwanakamati wa mambo ya *Implementation*, nataka kupongeza kwa kima fulani cha hii Kaunti ya Kilifi katika kuona kwamba mambo ambayo tunajadili hapa Bungeni yanatekelezwa tukilinganisha na kaunti nyengine jirani hapa. Kuna sehemu chache kidogo ambazo sisi kama Wabunge tuendeleo kutilia mkazo lakini hata hivyo hatujaachwa nyuma sana kiupande wa kuona kwamba mambo yale ambayo tunayajadili yanatekelezwa. Asante sana mheshimiwa Spika. Mungu awabariki.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you very much. Let us now get the hon. Member Dickson Shaban to make his contributions.

Hon. Shaban: Asante sana mheshimiwa Spika kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza, nataka nimshukuru mheshimiwa Gavana kwa hotuba ambayo ilikuwa nzuri sana. Hotuba ambayo ilisomwa na mheshimiwa Gavana ni hotuba ambayo ilikuwa imeboba sana hata ukiangalia hicho kingereza ambacho kimetumika hapo ni kiingereza cha hali ya juu na inatukumbusha kwamba *in future*, ni lazima tuchague Gavana ambaye pia anaweza kuzungumza lugha kama hii kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Spika, mimi nataka nimpongeze Gavana alipozungumza kuhusiana na kwamba ataleta Mswada wa kuhamasisha umma; kwa Kizungu wanauita *Civic Education Bill*. Mheshimiwa Spika, Mswada huu ni muhimu sana. Utakapoletwa hapa na kupitishwa, basi itaweza kupatia watu wetu haki ya kuweza kupata habari na haki ya kuwawezesha kwamba waweze kujua ni mambo gani ambayo yatakuua yanaendelea katika Kilifi Kaunti na pia itaweza kuwarahisisha watu kupata habari yoyote kuhusiana na kama ni miradi na habari za serikali kwa wananchi ili kuweza kusukuma gurudumu la maendeleo ya Kaunti ya Kilifi .

Pia nataka nimshukuru Bw. Gavana alipozungumza ya kwamba katika jimbo letu la Kilifi ni miongoni mwa jimbo ambalo liliweza kutunukiwa takriban shilingi million 6.4 ambazo kaunti 18 zilipata pesa hizo. Sisi tutaweza kufaidika na nina hakika zile pesa tumepata zitaweza kuboresha maendeleo kwa jimbo letu na hili lilitokea kwa sababu tuliorodheshwa kama jimbo ambalo limepiga hatua katika kukusanya ushuru.

Pia Mheshimiwa Spika, nataka nimpongeze tena kwa sababa kuna miswaada ambayo inakuja ambayo ni *Animal Disease Control Bill*, *Fisheries Management Development Bill*, *Agricultural Licensing Bill* na *Horticulture Development Bill*. Ikiwa Miswaada hii itakuja hapa Bungeni, nataka kusema tutakuwa na kazi nyingi lakini ikipita tutaweza kuboresha mambo ya kilimo na uvuvi katika jimbo letu la Kilifi.

Mheshimiwa Spika, la mwisho ni kwamba ni masikitiko kwamba Mheshimiwa Gavana anamaliza hatamu yake ya uongozi lakini ikiwa inawezekana kubadilisha Katiba, basi angetosha hata kwenda kipindi chake cha tatu kwa sababu ya kazi yake nzuri. Kwa hivyo, ninataka niunge mkono hotuba ya Mheshimiwa Gavana kwa sababu ni hotuba ambayo ililenga sekta zote ambazo yeye mwenyewe anaziwakilisha ili kuhahakisha kwamba mkaazi wa Kilifi anapata haki yake. Kwa hayo machache, nasema asante sana.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you. Hon. Thaura, please proceed.

Hon. Thaura: Thank you Mr. Speaker. I wish to stand in my capacity as the Chairperson for Heath Committee which is one of the most crucial Committees in this honourable House. I

would like to first appreciate our Governor for coming to this honourable House and give out his speech.

(Hon. Ziro stood on a Point of Order)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes hon. Peter Ziro, what is your Point of Order?

Hon. Ziro: Thank you Mr. Speaker. Is the Member in order if he can address himself as a Chairperson and we know all of us are hon. Members here?

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): But he is Chairperson of the Health Committee.

Hon. Ziro: But is he in order?

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): He is very much in order.

Hon. Ziro: Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Proceed.

Hon. Thaura: Mr. Speaker, he is a good friend of mine; so do not worry about him. I am the Chairperson and a very important Chairperson in this House.

(Laughter)

(Hon. Mramba stood on a Point of Order)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): There is a Point of Order from hon. Mramba. What is your Point of Order?

Hon. Mramba: Mr. Speaker, the Member on the Floor is uttering words that are not clearly understandable. Can he please clearly elaborate by the words “very important Chairperson”, does it mean there are other Committees which are not important in this Assembly?

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Please take your seat hon. Mramba. You should be guided that health is very important and he looks at the health of all the people in Kilifi County.

(Laughter)

Hon. Mramba: Mr. Speaker, I believe all Committees are equally important so the hon. Member is saying that the Health docket is more important than others; we need to know from the Floor of this House?

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Even if you look at the allocation in the budget, it eats into a very big chunk in the Kilifi County Budget that indicates how important the Department is, hon. Member, please proceed.

Hon. Thaura: And I wish to remind him that tomorrow we have a very important engagement in this House.

(Laughter)

Mr. Speaker, I listened to the Governor and ...

(Hon. Mumba stood on a Point of Order)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes hon. Mumba, what is your Point of Order?

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. Mumba: It is a Point of Information.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Do you wish to be informed?

Hon. Thaura: Yes please.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you.

Hon. Mumba: Yes indeed Health is a very important docket and as a Member to the Committee, I want to share this with hon. Members. Even in the Holy Book, there are Ten Commandments but there is one which has a promise; doesn't that signify that it is more important than the rest? It is when you respect your parents that you live long on this earth. It is very much in order that there are Committees which have more weight than the others. Health is universally a very crucial Committee in this House. Thank you.

Hon. Thaura: I listened to the Governor and there are things that I am worried about. As the Chairperson and representative of people of Sokoke, I looked at the ratio of the health workers on page 14; for those who have the copy of the speech. We have a deficit of nurses. The ratio of nurses is 40 to 100,000 and nationally the standard ratio should be 166 against 100,000 citizens. In the World Health Organization (WHO) it is 356 nurses against 100,000 citizens. I think we have a deficit and this is nothing to be proud of. As a County, we still have something to do. My wish is we have to look at the budgetary allocation and how it is prioritized in terms of the use.

I was also looking at the budgetary allocation in terms of pharmaceutical and non-pharmaceutical things we buy for the Department. I still believe though I am really happy that in our tenure as a Committee, we have improved in the Department. Actually, we have pushed the Department to an extent that when we came in as a Committee, the Department had pending bills of over Kshs80 million, but as we speak, Members you can bare me witness that we have drugs in the hospitals because we have been doing a commendable job. But again, as the Health Services Committee, we should increase the allocation that goes to the buying of pharmaceuticals and non-pharmaceuticals. So Mr. Speaker, I do commend the good job that the Governor is doing but I still feel we still have a lot to do in the Department of Health. Thank you, Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you. Hon. Abdul Omar Mohamed. Members you can now make a request; the system is now okay.

Hon. Omar: Asante sana mheshimiwa Spika. Nasimama kuuunga mkono hotuba ya mheshimiwa Gavana kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, mheshimiwa Dele. Mheshimiwa Spika, hii hotuba imegusia mambo mengi lakini ningependa kuzungumza kuhusu swala la ardhi. Mheshimiwa Spika, katika kipindi chake cha kwanza, kwa hakika Gavana aliweza kufaulu na kuhakikisha amepeana makao ama vyeti vya ardhi (*Adjudication schemes*) takribani 45 ambazo ni miradi iliyofanikiwa katika kipindi chake cha kwanza.

Mwaka huu alipofanikiwa kuingia katika kipindi chake cha pili, aliweza kupeana *allotment letters*. Hizi ni stakabadhi ambazo alizitoa katika maeneo ya Ukombozi na Matundo katika Kilifi Kaunti. Saa hii wanapanga kuleta *spatial plans* ambazo zinaletwa katika Kamati yetu ya Ardhi kisha baadaye zije Bunge na kupitishwa kwa manufaa ya wakaazi wa Kilifi.

Lengine ni kwamba kuna mradi uliofadhiliwa na Benki ya dunia ili kurudisha hadhi ya miji yetu ya Kilifi na Malindi mpango unaojulikakana kwa kizungu kama *Municipalities*. Hii itasaidia pakubwa maana tunajua kwamba serikali kuu inapanga kukatiza baadhi ya huduma zikiwemo mafuta ya taa kwani kufikia mwaka 2020 maswala ya mafuta ya taa yatakuwa hayatumiki tena katika miji yetu.

Sasa katika ufadhili huu kupitia *World Bank* ambapo itakuwa inaongozwa katika *Municipalities*, zitaweza kusaidia katika ule mfumo unaojulikana kama *Bio-gas*... mashimo yetu ya vinyesi tutaweza kusaidia wale wasiojiweza kupata umeme.

Pia, katika uhamasishaji wa ukataji miti wakati tu wa nyuma, serikali ilifungia misitu watu wetu wengi waliteseka kutokana na ukosefu wa makaa. Serikali ya Kilifi iweze kununua vifaa na kubadilisha takataka na kuzitengeneza kama makaa ili tuweze kujimudu katika hali kama hiyo.

Bw Spika, mbali na hayo kuna mengi ambayo yatasaidia manufaa kwa sababu kuna maeneo ambayo yamepangiwa kupatiwa *allotment letters* kukuza miji yetu ambayo sasa imetoka mbali kufikia sasa na serikali yetu pia itapata pesa kupitia *revenue collection* tunapolipia mashamba yetu.

Kwa hivyo, ningependa kumalizia hapo na kuunga mkono hii hotuba ambayo ina maelezo ya busara na hekima ambayo yataweza kufaidisha watu wetu wa Kilifi kwa ujumla. Asante mheshimiwa Spika.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you, hon. (Ms) Carol Kalume please proceed.

Hon. (Ms.) Carol: Thank you, Mr. Speaker for giving me this opportunity to give a feedback on the Governor's Address. First and foremost, I would like to congratulate His Excellency on his First Address of the Second County Assembly. His Address covered the challenges we have encountered as a county, the opportunities we came across and more successful programmes we have had. It also covered what is ahead of us.

Mr. Speaker, Sir, the people of Kilifi are anxiously looking to us as legislators to fully represent their interests and develop this County to their expectations. We have confidence in his Address because he had displayed excellent leadership skills and we are hopeful through working together with all stakeholders and the people of Kilifi we shall deliver and leave a legacy in accomplishing the programmes and projects envisaged in the 2018/2022 CIDP.

Mr. Speaker, Sir, the Kilifi CIDP 2018/2022 anchors on National Policies and Plans as well as international agenda. This presents to the people of Kilifi an opportunity to build on the game plan. This is a very same plan. It also provides a developmental road map for our County...the consensus on programmes and projects and the County Government committed to implement.

His Excellency the Governor touched on matters...

(Hon. Ziro stood on a Point of Order)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes, what is your Point of Order?

Hon. Ziro: Mr. Speaker, is the hon. Member giving a speech because it seems she is reading from somewhere? Please, guide us.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. (Ms) Carol, please can you read and address the concerns addressed by...

Hon. (Ms) Carol: Mr. Speaker, Sir, there is no difference at all because I took my time to sit down and analyzed the speech and because I want to articulate it in every aspect that was addressed by the Governor in my comfort to go through what I have....

(Hon. Hassan stood on a Point of Information)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes Hon. Hassan.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

Hon. (Ms.) Carol: Mr. Speaker, I do not want to be informed. I want to conclude what I have started.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you very much. Hon. (Ms) Carol, guided by the Standing Orders that we have, you can only quote or refer to an item by going through but otherwise you are supposed to make your contributions based on how you have been able to understand the speech by His Excellency, the Governor.

Hon. (Ms.) Carol: Thank you Mr. Speaker for the guidance and I shall be referring to what the Governor's address had articulated. Mr. Speaker, Sir, His Excellency, the Governor, also touched on matters fighting poverty, eradicating diseases, ensuring food security and improving access to clean and safe water.

Mr. Speaker, Sir, I really like to comment on the Department of Water giving my Ward, Mwawesa, the first point on bringing the water rig. As we are speaking, three boreholes have been dug and this has really improved the hard times our women had been going through walking more than three kilometers to look for water.

Mr. Speaker, Sir, I really support and concur with the Governor's Address because most of the issues affecting the common *Mwananchi* in Mwawesa and Kilifi at large were able to be addressed and well articulated. Thank you so much Mr. Speaker.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): The hon. Member for Garashi. Hon. Peter Ziro.

Hon. Ziro: Thank you, Mr. Speaker, for giving me the opportunity to contribute in support of the Governor's speech. I want to commend the Governor for his brilliant language in articulating issues that affect the county of Kilifi. I am happy because he started by recognizing the County Assembly as the pillar of democracy in the devolved government system. If you go to the Bible in the Lord's Prayer, Jesus ordered his disciples to say "Our Father who art in Heaven hallowed be thy name..." that means you start by giving praise to your creator. In this situation, the Governor has recognized the County Assembly as the epitome and pillar of democracy in the devolved governance of this country. I say God bless and long live the Governor!

He went ahead to emphasize on the issues of fighting poverty, improving education standards in the county, eradicating diseases, food security, access to roads and clear water amongst others. Mr. Speaker, we saw when flood affected our areas especially Adu and Garashi, we had plenty of food that was circulated out there showing that he is not a man of words but action. He has acted in providing some of these services to our people.

He has also talked of providing an enabling environment for businesses and tourism and being the Chairperson of Trade and Tourism at the County Assembly of Kilifi, I feel that I have been a bit lifted to know that the Governor is supporting tourism and the issue of providing soft loans to members of this county so that they can enhance themselves in terms of financial activities. We have the Mbegu Fund that is already in place. In fact, we are just waiting for a few things so that we can start distributing money to our people in Kilifi.

Mr. Speaker, Kilifi is rated the first with the highest developing expenditure absorption at a rate of 53 percent and this is according to the Report that was issued recently by the Controller of Budget. I do not know if the hon. Members are awake because they should be applauding this. This is a gesture to our County Government of Kilifi. It has not happened anywhere and it should go to the books of history. I applaud the Governor for his endless efforts in trying to make sure that projects in the county are being completed and they are given funding. He also hinted that he is engaging the World Bank in automating additional revenue streams...

(Hon. Mramba stood on a Point of Order)

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Kindly make your intervention. Proceed.

Hon. Mramba: Mr. Speaker, the Member on the Floor is referring to a Report by the Auditor General but as far as I am concerned, the latest report is contained in yesterday standard newspapers that exposed 22 most wasteful counties and Kilifi is one of them. So which latest report is he referring to?

(Applause)

Hon. Ziro: Thank you Mr. Speaker. I think the Member is misguided because this speech was read before yesterday, and he is talking of a newspaper that was printed yesterday. I am contributing in accordance with the speech here. Maybe English might be a problem to him.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Proceed. Yes Hon. Mramba what is it?

Hon. Mramba: Mr. Speaker, it is the hon. Member for Garashi who has earlier claimed that the source of that information was the latest Report of the Auditor General. I was only reminding him that the latest Report is contained in yesterday's Standard newspaper that says that Kilifi County is one of the 20 most wasteful counties. So which latest Report is he referring to, because the latest Report is contained in yesterday's standard newspaper?

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Mramba, the Member has been very clear as to state that he is referring to the Governor's address. So whatever was latest by then ...

Hon. Kiraga: Point of information!

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Would you wish to be informed?

Hon. Ziro: No!

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): He does not wish to be informed. Proceed.

Hon. Ziro: Mr. Speaker, I did not want to be informed but because he is senior to me, let him inform me.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): I have already taken a decision; you said you did not want to be informed.

Hon. Ziro: I want to remind my junior here hon. Mramba, when I call him *junior* I do in terms of education because I have not known hon. Mramba for stammering. He is very fluent but when he was talking, he was stammering and that implies that he has not understood whatever I was telling him...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Member for Garashi, please take your seat. There is a Point of Order from hon. Mumba, yes what is your Point of Order?

Hon. Mumba: Thank you Mr. Speaker. This is a House guided by facts and for purposes of records we need to get the facts straight. If we base on the speech given by the Governor and urge that we are going to debate on it and play dumb on the latest report the hon. Member from Kakuyuni is trying to bring before this House, then I think we are losing the meaning of power of current affairs. It is important we give our people what is currently happening. For purposes of clarity, I wish to say that we be guided and follow the latest Report so that our people can know what is trending.

(Hon. Kiraga stood on a Point of Information)

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Ziro, would you wish to be informed?

Hon. Ziro: Yes.

Hon. Kiraga: Thank you so much Mr. Speaker. I wish to inform the hon. Member for Garashi that this is a speech made by the Governor and it is prone to investigation to the issues

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

highlighted in those Departments and they are also prone to see whether they marry the correct situation on the ground and that is why when we are debating, it is not a matter of saying it is there; it has been highlighted by the Governor. No! We have to know, does this issue which has been highlighted marry with what is on the ground? Thank you very much.

Hon. Ziro: Thank you for the information hon. Kiraga. Mr. Speaker, I wanted to go ahead and explain or rather contribute and say that there has been a revenue shortfall and leakage in Kilifi County caused by Rain Drops Limited. Mr. Speaker, according to the Governor's speech; and I have been informed here that it was subject to verification under fact finding that the Governor has put in place mechanisms of trying to stop loss of revenue through cess and parking fees. He has placed personnel in every station to make sure that there is proper transparency and accountability and this, Mr. Speaker, if it works is going to help this county so that we can realize proper revenue collection.

Mr. Speaker, the Governor's speech has also focused on improving return on investing through marketing and value chain development. This is very important especially to the Tourism Sector which forms the backbone of this county.

Mr. Speaker, the Governor's speech promulgates the provision of affordable credit facilities and promoting fair trade practices in the County of Kilifi. This, Mr. Speaker, we have seen clearly because there are laws that are about to be enacted by my Department and as the Chairperson of the Committee on Trade, Economic Planning and Tourism, we are just about to bring to this honourable House five very important Bills that when enacted will help this County of Kilifi go to the standards which we are supposed to be in terms of Trade and Tourism. The Bills are; Trade and Market Bill, the Investment and Development Bill, Weight and Measures Bill, Beach Management Bill and Corporative Societies Bill.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Mramba, am I seeing an intervention?

Hon. Mramba: No! No!

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you. Proceed.

Hon. Ziro: So, Mr. Speaker, I want to wind up by saying that the speech has covered the Department that I Chair very effectively. We are just waiting to see the implementation of every aspect that has been mentioned in this particular speech. With those few remarks, Mr. Speaker, I wish to rest my case in support of the speech. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. (Ms.) Loice Ngari, is it an intervention or you want to make your contribution?

Hon. (Ms.) Ngari: Asante mheshimiwa Spika kwa kunipatia hii nafasi. Nami nataka kuongea kuhusu hotuba ya mheshimiwa Gavana. Ndani ya hotuba yake, mna kipengee kinachoangazia kuhusu dhuluma za kijinsia. Mheshimiwa Gavana ameangazia kuhusu usawa wa kijinsia kwamba amejizatiti kabisa hamsini kwa hamsini, na ili tuweze kuendelea na huu usawa ni kwamba dhuluma za kijinsia Kilifi Kaunti zimekithiri hususan kwa watoto wetu wasichana na imeweza kurudisha nyuma viwango vya elimu. Hivyo basi, kulingana na hotuba ya mheshimiwa Gavana, ameangazia kuwa kutakuwa na hamasa.

Mimi mheshimiwa Spika, nataka kuunga mkono hamasa hizi ambazo zitaenda kuangaziwa kulingana na hizi dhuluma na ili tuweze kuongeza viwango vya elimu ndio tuweze kupata ule usawa wa kijinsia hamsini kwa hamsini ni tuhakikishe kwamba wasichana wetu wameweza kusoma kikamilifu. Na ili waweze kupata taaluma nzuri, ni tuhakikishe kwamba hizi dhuluma zimekomeshwa. Kwa hivyo, ndani ya hotuba ya mheshimiwa Gavana mimi nataka kuunga mkono kabisa kuhusu hamasa hizi ambazo zitaenda kutekelezwa ndani ya Kilifi Kaunti ili tukaone kwamba wasichana wetu pamoja na vijana wetu wamepata haki zao za kimsingi. Asante sana mheshimiwa Spika.

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Yes. Hon. George Baya, please proceed.

Hon. Baya: Thank you very much Mr. Speaker, Sir, for giving me this opportunity to make my contribution. First of all, I am standing in support of the Governor's speech. There are two or three issues that touched on my Department.

Mr. Speaker, Sir, first of all as the Chairman for Public Investment and Accounts Committee, I am very interested in the mechanism or the proposal the Governor has made on controlling the revenue collection. This will help this County Government and save all the challenges which we have been encountering since devolution.

Second, there are plans the Governor has highlighted that he is going to upgrade the Kilifi General Hospital to Level 2 Mr. Speaker, Sir. This is going to help this County Government to reduce the cost of ambulance because most of our patients here when they need services, they have to go to Mombasa Hospital. So if we upgrade Kilifi Hospital to Level 2, it will help our people. Mr. Speaker, Sir, in his Excellency the Governor's speech....

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): There is a Point of Order from hon. Albert Kiraga.

Hon. Kiraga: Thank you so much Mr. Speaker. Can the Member on the Floor explain to us, what it entails for a Government hospital to be elevated to Level 2 facility? I believe Kilifi County Hospital is in level 4 which is now to be upgraded to Level 5 and he is talking of Level 2.

Hon. Baya: Thank you Mr. Speaker, Sir. Sorry it was a slip of the tongue but I meant...

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Hon. Thaura, what is your intervention?

Hon. Thaura: I would like to inform the hon. Member for Watamu.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Do you wish to be informed by the hon. Member who is also the Chairperson Health?

Hon. Baya: Yes.

Hon. Thaura: Thank you. Level 1 in the Health Sector is ...*(inaudible)*

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Proceed.

Hon. Baya: Thank you very much. As I already explained, it was just a slip of the tongue. Thank you for correcting me. I meant Level 5. Another thing in his speech the Excellency the Governor mentioned is the plan of reviving the cashew nut plant Mr. Speaker, Sir. If this Plant is revived, it will create a lot of job opportunities and also will bring back our cashew nut crop to its value. With those few remarks, I praise the Governor's speech. Thank you.

The Deputy Speaker (Hon. Kenga): Thank you. We are now moving to Mtepeni Ward. Hon. Member, please make your contributions.

Hon. Gogo: Asante Mheshimiwa Spika kwa nafasi hii uliyonipa ili nichangie machache kulingana na hotuba ya Gavana wetu. Kwanza, naipongezi hotuba yake na pia nikiwa mmoja wa wanakamati wa Ardhi. Mwenyekiti mdogo wa Ardhi amesimama na akaongea machache lakini mimi kama mwakilishi wa wadi ya Mtepeni, nasimama kwa niaba ya watu wangu.

Nilimsikiza Gavana vizuri sana na Mheshimiwa Spika, Ripoti inasema kuna mapande 45 ambayo yamefanyiwa vipimo na kati ya haya 45, kwa kipindi cha miaka mitano, ni mapande matano peke yake ambayo serikali yetu imepeana hati miliki. Hapo chini amesema ya kwamba kuna *alloyment letters* 1,200 ambazo kulingana na Ripoti zinasema zimepeanwa kwa Ukombozi na Mwatundo. Nataka nikujuze ya kewa Ukombozi na Mwatundo zinatoka ndani ya Wadi yangu ya Mtepeni.

Nikisimama kwa niaba ya watu wa Mwatundo, nataka niseme hapo mahali ambapo hizi barua zilitolewa kuna kesi inaendelea mpaka leo na ni wananchi wangu ambao kila siku wako kortini kutafuta sheria ya kupata ardhi hii ili waweze kuishi. Kile nilikuwa nataka nione mheshimiwa Gavana akipanga mipangilio, angetuelezea kama Bunge ile mikakati aliyonayo, kwa sababu hata haya mapande 45 ambayo amesema waliyafanyia *survey* ni zile ardhi ambazo

Disclaimer: *The electronic version of the Official Hansard Report is for information purposes only. A certified version of this Report can be obtained from the Hansard Editor.*

ziko chini ya Serikali Kuu. Kwa hivyo, hizi hazina shida. Unatumana kwa Idara ya Ardhi inafanya *survey* lakini ndani ya Kilifi Kaunti hata juzi waheshimiwa wenzangu nafikiri mlikuwa mashahidi. Diwani wetu alikuwa seli kwa sababu ya kesi ya mashamba. Nilikuwa natarajia Gavana angetupatia mwelekeo jinsi ambavyo tutawasaidia watu wa Kilifi wale ambao ni maskwota kununua hizi ardhi.

Ningeomba Bunge hili tafadhali ikiwa inawezekana Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi kuweka sheria ambayo tunamruhusu Gavana kuachilia million 100 kila mwaka wa kifedha kununulia wananchi wetu mashamba, sidhani kama hiyo pesa tutakuwa tumeitupa kwa sababu juzi tulikuwa na tume ya NLC (*National Land Commission*) kwa Wadi ya Watamu. Na nilikuwa na Mwenyekiti mdogo wa Ardhi, Mheshimiwa Omar, yule *Commissioner* wa Ardhi Mbagaya alisimama akasema ikiwa kuna shamba lolote ambalo liko kortini, tume haiwezi kuingilia hilo shamba. Kwa hivyo, nitauliza waheshimiwa wenzangu ni mashamba mangapi ambayo wananchi wetu wanayapigania hayako kortini? Nafikiri mashamba yote yiko ndani ya korti.

